

## Namna Ya Kusimama Kwenye Mwisho Wa Neno

Ziko namna tatu za kusimama kwenye mwisho wa neno<sup>1</sup>. Iliyo ya msingi ambayo ndio tutakayoielezea hapa ni kusimama kwa sukuwn.

Maneno ya kiarabu kawaida ni aina nne; ima neno liwe mwisho wake ni lenye sukuwn, au *manswuwb* (fat-hah au fat-hatayni) au *majruwr* (kasrah au kasratayni) au *marfuw'* (dhwammah au dhwammatayni).

Linapoishia neno kwa sukuwn hakuna budi linaposimamiwa lisimamiwe kwa sukuwn yake ya asili mfano:

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْخَرْ

Ama litakapoishia neno kwa fat-hah, kasrah au dhwammah au tanwiyn za kasratayni na dhwammatayn, basi linaposimamiwa lisimamiwe kwa sukuwn, lakini anapoendelea msomaji hukmu yake itabaki kama ilivyo.

Inapokuwa ni tanwiyn ya fat-hah, yaan fat-hatayn hubadilika na kuwa Alif inayovutwa kwa haraka mbili kwa vile inageuka kuwa ni *الْمُدُّ الْعُوضُ* (Maddul-'Twadhw)<sup>2</sup>; mfano neno la *مُصَدِّقًا* litatamkwa '**muswaddiqaa**' badala ya '**muswaddiqan**'. Ama akiendelea basi hukmu yake<sup>3</sup> itabidi ifuatwe kutegemea na herufi inayofuatia.

---

<sup>1</sup> (i) Kusimama kwa sukuwn (ii) Kusimama kwa *ar-raw-m* na *ikhtilaas* (iii) Kusimama kwa *ish-maam*

<sup>2</sup> Rejea mlango wa Maddutw-twabiy'i

<sup>3</sup> Rejea mlango wa 'Nuwn saakinah na tanwiyn'

Matamshi ya herufi za mwisho katika kusimamia kwa sukuwn au kuendelea neno la kawaida		
Kusimama	Kuendelea	Neno
الْكَافِرِينَ al-kaafiriyn	al-kaafiriyna	الْكَافِرِينَ
الأَرْضُ al-ardhw	al-ardhwi	الْأَرْضِ
الْحَقُّ al-haqq	al-haqqu	الْحَقُّ
كَلِمَاتٍ kalimaat	kalimaatin	كَلِمَاتٍ
فَرِيقٌ fariyq	fariyqun	فَرِيقٌ

Matamshi Ya Herufi Za Mwisho Katika Kusimamia Au Kuendelea Neno Lenye ة		
Kusimama kwa ه	Kuendelea	Neno
ذُرِّيَّةٌ dhurriyyah	dhurriyyatan	ذُرِّيَّةٌ
قَرْيَةٍ qaryah	qaryatin	قَرْيَةٍ
مَغْفِرَةً maghfirah	maghfiratun	مَغْفِرَةً